OSHA
Occupational Safety and Health Authority

# JARIDA MTANDAONI

TOLEO MAALUM LA MAADHIMISHO YA USALAMA NA AFYA DUNIANI NA MEI MOSI | Tarehe 26/04 - 1/05/2023

## RAIS SAMIA: TUNAKWENDA KUIPANDISHA HADHI OSHA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwapungia mkono viongozi pamoja na Wafanyakazi mara baada ya kuwasili katika uwanja wa Jamhuri kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Sherehe za siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi ambapo Kitaifa zimefanyika Mkoani Morogoro tarehe 01 Mei, 2023.

TANZANIA YAADHIMISHA SIKU YA KIMATAIFA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI - UK 3

PROF. NDALICHAKO : SERIKALI YETU INATHAMINI MASUALA YA MASUALA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI - UK 4

OSHA YAAHIDI KUTEKELEZA MAONO YA RAIS SAMIA SULUHU KATIKA KUBORESHA USALAMA NA AFYA NCHINI.- UK 7

# RAIS SAMIA: TUNAKWENDA KUIPANDISHA HADHI OSHA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Profesa Joyce Ndalichako na Viongozi wengine wakiimba Wimbo wa Mshikamano (Solidarity) wakati wa Sherehe ya Mei Mosi Mkoani Morogoro tarehe 01 Mei, 2023.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa serikali imeanza mpango wake wa kuiimarisha taasisi ya OSHA na tayari imetoa watumishi 18 pamoja na magari 13 ili kurahisisha shughuli za usimamizi wa masuala ya usalama na afya katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini, Rais Samia ametoa kauli hiyo wakati wa hotuba yake katika kilele cha maadhimisho ya sherehe za mei mosi zilizofanyika Mkoani Morogoro

“Katika mwaka huu wa fedha 2022/23 tumefanya kazi nzuri ya kuiimarisha OSHA ambapo tayari tumewaongezea wafanyakazi 18 na magari 13 ili yawasaidie, tulianzisha chombo hiki mahususi cha usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi ilikusimia masuala husika na tupo katika mchakato wa kuwaongezea wafanyakazi iliwafanyanyekazizaovizuri” alisemaDkt.Samia

Aidha Rais Samia akijibu hoja ya Mkurugenzi Mkazi wa Shiriki la Kazi Duniani ILO, Wellington Chibebe kuhusu kuridhia mikataba pamoja na kurekebisha sheria na kanuni mbalimbali za kazi amemuhakikishia kuwa Tanzania imaenza kufanyia kazi swala hilo tangu muda mrefu.

“Tanzania imeanza kuridhia mikataba hiyo tangu muda mrefu mfano tumeandaa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi mwaka 2010 lakini tumeanzisha chombo mahususi cha serikali cha kusimamia masuala ya usalama na afya mahali pa kazi ambacho ni OSHA mwaka 2001 na leo kwa malalamiko hayo ya wafanyakazi tunakwenda kuipandisha hadhi OSHA kwa kuipa vitendea kazi pamoja na watumishi wanaostahili” aliongeza Rais Samia.

# TANZANIA YAADHIMISHA SIKU YA KIMATAIFA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (katikati) akiwaongoza Wageni wa meza kuu kupokea maandamano ya wafanyakazi kuingia katika Viwanja vya Tumbaku katika hafla ya Kilele cha maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi

Aprili 28, 2023 Tanzania imeungana na mataifa mengine ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa lengo la nikuendeleza kampeni za kuhamasisha uwepo wa mazingira salama na yenye kulinda afya za watu katika sehemu za kazi.

Maadhimisho hayo yamefanyika Kitaifa Mkoani Morogoro ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako huku yakihusisha shughuli mbalimbali ikiwemo Kaguzi na upimaji wa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa vyombo vya habari kama TBC, WASAFI MEDIA, CHANNEL 10 na UHURU FM, Maonesho ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaliyoanza tarehe 26 hadi Mei mosi, Mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi kwa Wajasiriamali wadogo, wafanyakazi wa viwandani pamoja na wachimbaji makaa ya mawe Pamoja na Shindano la Tuzo za usalama na afya mahali pa kazi. Akihutubia mamia ya wakazi wa Morogoro na washiriki wa shughuli za maadhimisho kutoka katika mikoa mbali mbali nchini Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako amesema kuwa lengo la maadhimisho ya siku hii nikuwahamasisha waajiri kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa magonjwa na ajali zinazotokea maeneo ya kazi.

Maadhimisho haya kwa mwaka huu 2023 yaliongozwa na kauli mbiu inayosema : Mazingira salama na afya ni kanuni na haki ya masingi mahali pa kazi huku yakikutanisha jumla la washiriki zaidi 100 kutoka makampuni mbalimbali na taasisi binasi na za umma .

# “SERIKALI YETU INATHAMINI MASUALA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako akihutubia Wafanyakazi waliojitokeza katika hafla za Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro katika Viwanja vya Tumbaku.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako amesema kuwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua na kuthamini masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwasababu ni haki ya msingi kwa kila mfanyakazi. Waziri Ndalichako ametoa kauli hiyo wakati akihutubia wakazi wa Morogoro Pamoja na wafanyakazi kutoka maeneo mbalimbali ya kazi nchini katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi. “Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kinara wa kuhakikisha kuwa nguvu kazi ya taifa inalindwa kwa kuhakikisha anaimarisha taasisi ya OSHA na kupitia OSHA Serikali imeendelea kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa Sheria Na 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003 na lengo ni kuhakikisha kuwa maeneo ya kazi yote nchini yanakuwa na mifumo Madhubuti ya kuwakinga wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali zinazoweza kuwapata katika maeneo yao ya kazi” alisema Prof.Ndalichako

# "TANZANIA IMEPIGA HATUA KUBWA KATIKA USIMAMIZI WA MASUALA YA USALAMA NA AFYA"




Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi Khadija Mwenda akitoa neno la utangulizi Pamoja na utambulisho wa wageni mbalimbali walioalikwa katika hafla ya kilele cha Maadhimisho ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi Khadija Mwenda amesema kuwa nchi ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi na imekuwa ni mfano kwa nchi nyingine kuja kujifunza namna ambavyo OSHA imesimika mifumo ya usimamizi wa masuala husika

Bi. Khadija ametoa kauli hiyo wakati akihutubia akihutubia katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi Mkoani Morogoro "Nchi yetu imepiga hatua kubwa sana katika masuala ya usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi na wenzetu nchi za Jirani wamekuwa wakija nchini kujifunza na kuangalia namna ambavyo tumeweza kusimika mifumo ya masuala ya usalama na afya katika maeneo ya kazi na hii yote inatokana na utashi wa viongozi wetu wa kuona kwamba afya ya usalama wa mfanyakazi ndio kipaumbele" Alisema Bi. Khadija Mwenda

# ILO YAIPONGEZA OSHA KWA KUWEKA MIFUMO DHABITI YA KULINDA WAFANYAKAZI NCHINI



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Bi Getrude Sima akitoa salam za maadhimisho kutoka kwa Mkurungenzi Mkazi wa ILO kwa Mhe. Waziri Ndalichako pamoja na wafanyakazi wote waliohudhuria hafla hizo.

Shirika la Kazi Duniani (ILO) limeipongeza Taasisi ya OSHA kwa kuendelea kuboresha mifumo ya usalama na afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika hilo, Bw. Willington Chibebe na kuwasilishwa na Bi. Getrude Sima katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi zilizofanyika Mkoani Morogoro katika viwanja vya Tumbaku.

“Napenda kuipongeza OSHA kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha usalama na afya katika maeneo yote ya kazi unazingatiwa, tunajivunia sana uwepo wa OSHA na tumekuwa tukishirikiana nao vizuri katika masuala mabalibali na hata hivi karibuni tumeshuhudia wenzetu kutoka nchi mbalimbali za jirani wakiwemo Kenya wakija kujifunza namna ambavyo OSHA imefanikiwa kuweka mifumo thabiti ya usalama na afya katika maeneo ya kazi.” alisema Bi. Getrude Sima kwa niaba ya Bw. Willington Chibebe.

Aidha Bw. Willington Chibebe amesema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye utendaji mzuri katika masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa ukanda wa Afrika Mashariki ambapo Shirika hilo linasiamamia nchi zote tano za Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi.

# OSHA YAAHIDI KUTEKELEZA MAONO YA RAIS SAMIA SULUHU KATIKA KUBORESHA USALAMA NA AFYA NCHINI.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (wa sita kushoto) na Wageni wa meza kuu wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa OSHA katika Viwanja vya Tumbaku wakati wa hafla ya Kilele cha maadhimisho ya Safety Day 2023

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umeahidi kuendelea kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuwezesha dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi nchini yanakuwa salama inatimia.

Kauli hiyo imeelezwa na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi. Khadija Mwenda, alipozungumza na Jarida hili kuhusu mpango wa Taasisi yake wa kuhakikisha kwamba dhamira ya serikali ya kulinda nguvukazi ya nchi inawekwa katika vitendo.

"Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi wetu wote wa juu katika Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwajali wafanyakazi wa Tanzania kama alivyoeleza katika hotuba yake ya Mei Mosi kwamba pamoja na kuanzisha Taasisi mahsusi ya kusimamia masuala ya Usalama na Afya, serikali yake inaendelea kuijengea uwezo OSHA kwa kuajiri watendaji wa kutosha na kuwapatia vitendea kazi muhimu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo," amesema Mtendaji Mkuu wa OSHA.

Katika hotuba yake ya Mei Mosi Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alielezea mpango wa serikali katika kuiimarisha Taasisi ya OSHA kwa kuiongezea rasilimali watu pamoja na vitendea kazi ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Taasisi hiyo.

# WAAJIRI WATAKIWA KUWEKA MIFUMO THABITI YA KULINDA WAFANYAKAZI WAO DHIDI YA AJALI NA MAGONJWA.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako akihutubia Wafanyakazi waliojitokeza katika hafla za Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro katika Viwanja vya Tumbaku

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako ametoa wito kwa waajiri na wamiliki wa maeneo ya kazi nchini kuhakikisha wanaweka mifumo stahiki ya kuwalinda wafanyakazi wao dhidi ya ajali na magonjwa katika maeneo yao ya kazi. Prof. Ndalichako ametoa wito huo wakati akihutubia katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi Mkoani Morogoro akibainisha kuwa suala la usalama na afya mahali pa kazi lisipo zingatiwa linaweza kusababisha upotevu wa Maisha ya wafanyakazi lakini pia kuathiri shughuli za uzalishaji

“ Nawakumbusha waajiri wote nchini kuhakikisha wanatimiza jukumu lao la msingi la kulinda usalama na afya za wafanyakazi wao kama yalivyo matakwa ya Sheria Na5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003, ni ukweli usiopingika kwamba ajali na vifo vinavyoweza kutokea kazini vinaweza kuzuilika kama hatua stahiki za kuzuia zitachukuliwa” alisema Prof. Ndalichako

# BI. KHADIJA: USALAMA NA AFYA USIPOZINGATIWA NI JANGA KIUCHUMI NA KIJAMII




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (kulia) na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi Khadija Mwenda wakipokea maandamano ya maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi . Khadija Mwenda amesema kuwa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yasipozingatiwa inaweza kupelekea janga kiuchumi na hata kijamii.

Bi. Khadija ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na mamia ya wafanyakazi na wakazi wa Morogoro katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro.

"Kila siku jumla ya wafanyakazi wapao 6,300 hupoteza Maisha kutokana na ajali au magonjwa yatokanayo ya kazi na jumla ya vifo milioni 2.7 pamoja na ajali milioni 374 hutokea kila mwaka duniani" alisema Bi. Mwenda akiongeza kuwa. "Endapo hapatakuwa na mifumo thabiti ya kumlinda mfanyakazi kunauwezekano mkubwa sana wa kuathiri uchumi na pato la taifa hivyo maendeleo hayawezi kupatikana hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi yanakuwa salama na yanaangalia utu wa mfanyakazi na hali ya kutafuta kipato isitumike kama sehemu ya kutomthamini mfanyakazi"

Aidha Bi. Khadija Mwenda akieleza hali ya utekelezauji wa masuala ya usalama na afya nchini amebainisha kuwa bado kunachangamoto na kupitia utafiti uliofanywa na OSHA sekta ya uzalishaji ilikuwa inaongoza kwa matukio ya ajali ikifuatiwa na sekta ya ujenzi pamoja na madini.

# WAZIRI NDALICHAKO: TUZO HIZI ZIKAWE CHACHU YA KUBORESHA MAZINGIRA YA KAZI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (kulia) akimkabidhi Meneja wa NSSF Mkoa wa Morogoro, Rose Meta (kushoto) tuzo ya ushindi wa jumla kwa Taasisi za Umma zinazotoa Huduma ya Hifadhi ya Jamii katika sekta binafsi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako amewataka wadau wote walioshinda tuzo za usalama na afya katika mwaka huu 2023 kuhamasika kufanya vizuri zaidi katika kuimarisha mifumo ya usalama na afya katika maeneo yao ya kazi.

Waziri Ndalichako ametoa kauli hiyo kabla ya kuhitimisha hituba yake kwa wafanyakazi wa maeneo mbalimbali ya kazi nchini katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi yaliyofanyika kitaifa Mkoani Morogoro katika Viwanja vya Tumbaku.

"Serikali kupitia taasisi ya OSHA imeanzisha tuzo kwa taasisi na makampuni yanayoonesha juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi, natumia nafasi hii kuwapongeza wote walioshinda tuzo katika vipengele mbalimbali kwa mwaka huu 2023 lakini pia niwakumbushe washindi wote isiwe sasa mgema akisifiwa tembo hulitia maji nimatumaini yangu sasa tuzo hizo zitakwenda kuwa chachu ya kuboresha mazingira ya usalama na afya kwa wafanyakazi wenu" Alisema Prof. Ndalichako

# MATUKIO KATIKA PICHA

## MAADHMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI 2023




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako akisalimiana na Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, Mhe. Dkt. Yose Joseph Mlyambina



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),Prof. Jamal Adam Katundu akizungumza na wafanya-kazi kutoka maeneo mbalimbali ya kazi wakati wa hafla za kilele cha maadhimisho ya usalama na afya Duniani.




Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya OSHA (MAB), Dkt. Adelhelm Meru akitoa neno la shukrani kwa Mhe. Waziri Prof. Joyce Ndalichako (hayupo pichani), wageni waalikwa pamoja na wafanyakazi wote waliojitokeza katika hafla za kilele cha maadhimisho ya usalama na afya Duniani.



Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi Khadija Mwenda akitoa neno la utangulizi Pamoja na utambulisho wa wageni mbalimbali walioa-likwa katika hafla ya kilele cha Maadhimisho ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri (ATE), Bi. Suzanne Ndomba-Doran akizungumza kuhusu mkikakati ya chama cha ATE ya kushirikiana na OSHA katika kutoa mafunzo kwa waajiri na wafanyakazi



rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhokya akizungumza na wafanyakazi katika hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## MAADHMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Bi Getrude Sima akitoa salam za maadhimisho kutoka kwa Mkurungenzi Mkazi wa ILO kwa Mhe. Waziri Ndalichako pamo-



Bendi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT-Brass Band) ikiongoza Wafanyakazi kutoka Maeneo mbalimbali ya kazi katika maandamano yalionazia katika Soko Kuu la Chief Kingalu mpaka katika Viwanja vya Tumbaku - Morogoro



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako akikabidhi tuzo kwa moja ya washindi walioshinda tuzo hizo za usalama na afya mahali



Wafanyakazi kutoka Maeneo mbalimbali ya kazi wakifuatilia hotuba kutoka kwa viongozi mbalimbali wakati wa hafla za kilele cha maadhimisho ya siku ya usalama na afya mahali pa kazi Duniani



Msanii wa muziki Peter Msechu akitoa burudani katika kilele cha maadhimisho ya siku ya usalama na afya mahali pa kazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Mkoani Morogoro.



Kikundi cha Ngoma za asili kikitoa burudani katika kilele cha maadhimisho ya siku ya usalama na afya mahali pa kazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Mkoani Morogoro.

# MAADHIMISHO YA MEI MOSI

WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA) WAUNGANA NA WAFANYAKAZI WENGINE KUTOKA MAENEO YA KAZI MBALIMBALI NCHINI KUADHIMISHA MEI MOSI KITAIFA MKOANI MOROGORO KATIKA UWANJA WA JAMHURI, 1/05/2023










**OSHA TANZANIA**

**Wakala Wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi,**
**P.O.Box 519,**
**Dar es Salaam**
**Phone : +255-22-2760548**
**Email Address : info@osha.go.tz**
**Simu bure: 0800110091/2**
**Websites: www.osha.go.tz**